

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI

21 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI – TAREHE 21 APRILI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

82. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Afya wa kutosha katika Kituo cha Afya Itaka.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

83. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga walau kilomita chache barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo mpaka Lumecha kilomita 296.

WIZARA YA MADINI:

84. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni lini uchimbaji wa Madini ya Dhahabu utaanza katika eneo la Utegi Tarafa ya Girango.

WIZARA YA KILIMO:

85. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzalisha Mbegu bora za Parachichi aina ya *Hass* na kuzigawa kwa Wakulima kwa bei nafuu.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

86. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Majengo ya Wizara ya Elimu Zanzibar ili kutoa huduma kwa wakati na kupunguza gharama za kukodi Ofisi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



**DODOMA
21 APRILI, 2022**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**